**Jina la Kitabu: Fungate ya Uhuru**
**Mwandishi: M.S. Khatib**
**Mhakiki: S.M. Sanka**

## Utangulizi

*Fungate ya Uhuru* ni diwani yenye mkusanyiko wa mashairi 45 yenye urefu tofauti. Mashairi yaliyomo katika diwani hii pia yanatofautiana kimtindo. Tutazingatia tofauti hizi katika uchambuzi wetu. Tutaanza kuvichambua vipengele vya fani na kisha vipengele vya maudhui.

Katika uchambuzi wa fani tutatazama uhusiano wa jina la kitabu na yaliyomo, miundo ya mashairi, na matumizi ya lugha. Kisha tutatoa tathmini ya ufundi wa mshairi katika kuumba sanaa yake. Uchambuzi wa maudhui utazingatia dhamira, migogoro, ujumbe na maadili, na falsafa ya mshairi. Hatimaye tutafanya tathmini ya falsafa ya mwandishi na maadili yake katika kushughulikia migogoro anayozungumzia.

## Jina la Kitabu

Diwani hii inaitwa *Fungate ya Uhuru*. Jina hili liahusiana sana na yaliyomo katika kitabu. Ili tuweze kuona jinsi jina linavyohusiana na yanayozungumziwa katika kitabu tunapaswa kufafanua kwanza maana ya maneno **fungate** na **uhuru**.

**Fungate** ni kipindi cha siku saba kuanzia siku ya harusi. Kwa lugha ya Kiingereza hujulikana kama ***honeymoon***. Fungate inaweza kudumu zaidi ya siku saba ikiwa wahusika ni mabruki, yaani matajiri. Siku ya fungate ni siku za raha na starehe. Maharusi hufurahia muungano wao mpya. Kwa kawaida gharama za fungate huwa zinalipwa na ndugu, jamaa na marafiki wa maharusi. Endapo siku za fungate zitazidi inawezekana kabisa waliochangia wakakereheka.

**Uhuru** ni hali ya mtu, jamii, au taifa kuwa na uwezo wa kujiamulia mambo yanayohusu maisha yao. Kwa nchi zilizotawaliwa na wakoloni, Tanzania ikiwa mojawapo, tukio la kupata uhuru ni sawa na harusi. Uhuru husherehekewa kwa gharama za Kitaifa. Katika sherehe hizi wanaofaidi zaidi huwa ni Viongozi wa Serikali. Wananchi na viongozi wao wako katika uhusiano mpya unaoimarishwa na matumaini ya maisha bora. Kutokana na hali hiyo fungate inapodumu muda mrefu wananchi, ambao ndio wanaobeba gharama, huanza kunung'uika.

Hivyo *Fungate ya Uhuru* ni diwani yenye mashairi ambayo baadhi kubwa yanabainisha hali za wananchi wa nchi za kiafrika baada ya uhuru. Wananchi hao wanajiona kuwa kiu yao ya maendeleo, uhuru na haki haijazimwa wakati viongozi wao wakiendelea na fungate kwa gharama za wananchi haohao.

**Muundo.**

Muhamed Seif Khatib katika *Fungate ya Uhuru* ametumia mchanganyiko wa miundo mbalimbali ya mashairi ya kimapokeo. Miundo aliyotumia ni mingi sana kiasi kwamba hatuwezi tukabainisha yote katika safu hii ndogo. Hata hivyo tutatoa mifano michache ya miundo inayojitokeza sana katika diwani hii.

**Mashairi ya Uwili.**

Mashairi ya uwili ni yale ambayo yana muundo wa mistari miwili miwili kwa kila ubeti. Mfano wa shairi la uwili katika diwani hii ni "Mjamzito" (uk. 8). Katika shairi hili mstari wa kwanza una mizani 12 na wa pili una mizani 8. Tazama beti tatu zifuatazo:

Mjamzito, amelazwa "thieta"!
Lazima apasuliwe,

Chake kitoto, tumboni kinatweta,
Hawezi kujifunguwa,

Mwili u moto, tumbo linamkeketa,
Kwa kite anaunguwa.

Mashairi ya uwili siyo mengi katika kitabu hiki. Inaelekea mshairi hapendelei sana muundo huu. Hata hivyo inawezekana mashairi ya uwili ni vigumu zaidi kuyatunga kwa sababu ya ugumu wa kupata utoshelevu katika mistari miwili tu.

**Mashairi ya utatu**

Mashairi ya utatu yanajitokeza kwa kiasi fulani katika diwani hii. Haya ni mashairi ambayo yana mistari mitatu mitatu katika kila ubeti. Mashairi ya utatu katika kitabu hiki ni pamoja na "Fungate" (uk. 1), "Sikubimbi" (uk. 48), "Paka Shume" (uk. 49), "Wewe peke yako" (uk. 49-50), "Nia yangu sigeuzi" (uk. 50) na "U wapi uzuri wako". Mashairi haya yana vibwagizo vyenye mstari mojamoja. Lakini mashairi ya "Nia yangu sigeuzi" na "sikubimbi" yana vibwagizo vyenye mistari miwili. Hapa chini tutatoa mifano miwili ya kila kundi:

"Sikubimbi"

Ukiwa wewe jeuri, Safini wa kutamka,
Utanikuta jabari, kwa hilo nimesifika,
Wala huna uhodari, mtegoni umefika,

Kibwagizo:-
Umelichimba kaburi, mzima utajizika.
Huna tena ujasiri, sikubimbi umefika.

"U wapi uzuri wako"

U wapi uzuri wako, haupo umepoteya,
Yawapi maringo yako, na hashuyo za duniya,
Leo upo peke yako, sote tumekukimbiya,

Kibwagizo:-
U wapi uzuri wako, ya wapi maringo yako.

Mashairi haya ya utatu yakibaki bila kibwagizo yanaweza kuwa ni ya aina ya utatu, lakini kibwagizo ni sehemu muhimu katika tungo hizi. Hivyo tunaweza kusema kuwa katika diwani kuna ushairi wa aina nyingi kama tulivyoonesha katika mifano hapo juu.

**Mashairi ya Unne.**

Muundo wa mashairi ya unne umezoeleka sana katika ushairi wa Kiswahili. Mashairi ya unne yana mistari minne minne katika kila ubeti. Katika kitabu hiki mashairi ya unne ni pamoja na:

"Kuntu sauti ya Kiza" (uk. 36)
"Mcheza Hawi Kiwete" (uk. 41)
na
"Ua si Ruwaza Jema" (uk. 51-52)

Tazama mfano ufuatao kutoka katika shairi la "Mcheza Hawi Kiwete";

**Mcheza Hawi Kiwete**, Kilema kilomshika,
Lau mcheza wa Kete, angezila pasi shaka,
Au kama kibafute, ushindi angeushika,
Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao.

Ngoma yataka matao, huchezwa kwa kudemka,
Kwa maringo na pumbao, mwili wote kunyumbuka,
Haichezwi kama bao, komwe zako kupangika,
Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao.

**Mashairi ya Utano.**

Haya ni mashairi yaliyo na mistari mitano mitano kwa kila ubeti. Katika diwani hii mashairi ya ina hii yamejitokeza kwa kiasi kidogo. Mashairi ya utano ni pamoja na **Ladha ya Maji Katani**" (uk. 39), "Unganeni" (uk. 2) na "Nimekuwa na Sauti" (uk. 11-12): (Shairi hili limetungwa na Jumanne Mayoka).

**Mashairi ya Usita.**

Haya ni mashairi ambayo yana mistari sita sita katika kila ubeti. Mashairi ya aina hii nayo siyo mengi sana. Shairi la usita katika diwani hii ni "Dafina" (uk. 9-10). Tazama mfano wa beti hizi mbili:-

1. **Paa, ni kuruka angani, kama ndege na tiara**
   **Paa, ni mnyama porini, ni mwenye nyingi papara,**
   **Paa, ni kuteka mekoni, moto uwake imara,**
   **Paa, ni magambani, samaki atiye sura,**
   **Paa, ni la nyumbani, makuti au karara,**
   **Mgodi wa Kiswahili, ni dafina isokwisha.**

2. **Kata, ni kulikata kuti, kwa panga au kitara,**
   **Kata, ni kunjio la kati, umbo la nyoka duwara,**
   **Kata, ni kujitwika mti, unajiweka tambara,**
   **Kata, ni kiponya mauti, kiu inapocharura,**
   **Mgodi wa Kiswahili, ni dafina isokwisha.**

Hata hivyo shairi hili lina mistari mitano mitano katika baadhi ya beti zake kama inavyoonekana katika mfano hapo juu. Katika jumla ya beti tisa za shairi hili beti mbili zina mistari mitano mitano. Beti zingine zilizobaki zina mistari sita sita.

**Mashairi ya Unane:**

Mashairi ya aina hii ni yale yenye mistari minane minane kwa kila ubeti. Katika kitabu hiki kuna shairi moja tu la aina hii. Shairi hili ni "Nchi Yangu" (uk. 6).

Mashairi yenye beti zenye mistari mingi siyo mengi katika kitabu hiki. Shairi la "Mkata" (uk. 20-22) lina mistari 11 na 12 katika baadhi ya beti zake tano.

Jambo linalodhihirika katika diwani hii ya Muhamed Khatib ni kwamba hakuna muundo wa aina moja unaotawala katika mashairi yake. Kuna miundo na mitindo ya aina mbalimbali. Miundo mingi ni ile isiyoelezeka katika ushairi wa Kiswahili.

Hali hii inadhihirisha kwamba mshairi huyu ana ufundi wa hali ya juu sana wa sanaa ya ushairi. Tutatoa mifano michache ya miundo ya mashairi yake katika sehemu ifuatayo.

**Miundo Mingine**

Diwani ya *Fungate ya Uhuru* ina miundo mingi tofauti ambayo inaonekana mipya kwa wasomaji wengi. Tutazame mifano ifuatayo:

**Naona**

Shairi hili lina mistari sita katika kila beti zake. Wakati mistari minne ya kati ina mizani nane (8) kila moja, mstari wa kwanza unaundwa kwa neno moja lenye mizani tatu (3) na mstari wa mwisho una mizani sita (6). Tazama beti tatu za shairi hili:

*Naona*
*Jasho lawatiririka*
*Na majembe na mashoka*
*Wakulima wameshika*
*Mashamba yao kufyeka*
*Ni wachapa kazi!*

*Naona*
*Wakulima na magwanda*
*Nyonga zao wamepinda*
*Mazao yao kupanda*
*Ya nafaka na Matunda*
*Kazi ni Kilimo!*

*Naona*
*Mvua ziliponyesha*
*Mimea kurutubisha*
*Na jua likahuisha*
*Mazao kuyaivisha*
*Nyayo kutuliya.*

Muundo huu haufanani na miundo tuliyoizoea katika ushairi wa Kiswahili.

Ingawa Mohamed Seif Khatib amezingatia kanuni za ulinganifu wa vina na mizani, ameongeza miundo mipya. Hali hii inadhihirisha kwamba kanuni za kimapokeo za ulinganifu wa vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili hazimzuii mshairi kubuni miundo mipya. Shairi lifuatalo linaimarisha hoja hiyo.

**Kinyang'anyiro**

*Nyati lilipoangushwa viliingia vishindo*
*Vishindo vya Kufa na Kupona*
*Vishindo vya Kunyang'anyana*
*Kiteo*
*Ikawa Kupiganiana*
*Nyama ya Nyati alonona.*

*Palikuwa patashika kuanza kinyang'anyiro*
*Kinyang'anyiro cha kukaba*
*Kinyang'anyiro cha kuiba*
*Kiteo*
*Nyama ya Nyati alonona*
*Kishibisha yao matumbo.*

*Wasiokuwa wasasi wakafanya unyang'anyi*
*Unyang'anyi wa kupora*
*Unyang'anyi wa ngawira*
*Kiteo*
*Kushibisha yao matumbo*
*Siwafike wahusika*

Bila shaka wasomaji watakiri kuwa muundo huu ni mpya katika ushairi wa Kiswahili pamoja na kuzingatia ulinganifu wa vina na mizani. Wanafunzi wa somo la ushairi wanashauriwa kubainisha miundo mingine inayofanya diwani hii kutofautiana au kufanana na diwani za washairi wengine.

**Matumizi ya Lugha**

Mohamed Seif Khatib katika diwani hii ya **Fungate ya Uhuru** ametumia kwa kiasi kikubwa Kiswahili Sanifu. Tofauti na washairi wengi wa mwambao kama vile Shaaban Robert, Muhamed Khatib hakuonyesha athari kubwa ya lugha ya Kiarabu katika Mashairi yake.

Hata hivyo katika baadhi ya mashairi mwandishi ametumia lahaja za Kiswahili. Mathalani neno "**Mato**" badala ya "macho" **(Shairi la Mjamzito uk. 8).** Neno hili linatokana na lahaja ya Kimvita ambacho huzungumzwa Kaskazini wa mwambao wa Afrika Mashariki. Inaonekana kwamba lengo la mwandishi kutumia neno hilo ni pamoja na kupata ulinganifu wa vina kama inavyodhirika katika beti hizi zifuatazo:

**Mjamzito**

*Maji ya Moto, Na zana za Kukata*
*Mganga kasogezwa*
*Kawa mzito, Dakitari asita*
*Aogopa kupaswa*
*Na yake* ***mato****, machozi yanatota*
*Huruma yamsumbua.*

**Lugha ya Picha**

Mwandishi ametumia lugha ya picha kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya mashairi yamejengwa kwa taswira maalumu. Mathalani shairi la **Mjamzito** ni taswira ya matatizo ya wananchi ambapo dakitari, yaani Kiongozi wa Serikali, anashindwa kufanya upasuaji ili kunusuru maisha ya mjamzito. Upasuaji ni uamuzi wa Serikali ambao japo unaweza kuwa mgumu lakini ndiyo njia pekee ya kuwaondolea matatizo wananchi.

Mashairi yaliyojengwa katika taswira au picha maalumu yako mengi katika diwani hii. Tukitaja baadhi tu ni kama vile "Dafina" (Uk.9-10), "Nahodha Mtwesi" (uk. 7), "Kungwi" (uk. 28), "Ukasuku" (uk. 33), "Wingu" (uk. 39), "Paka Shume" (uk. 49) n.k.

Matumizi ya lugha za picha katika diwani hii yameshehenezwa kwa utajiri wa tamathali za semi. Tutazame mfano wa tamathali za semi katika shairi lifuatalo:

**U Wapi Uzuri Wako**

Uwapi uzuri wako, haupo umetoya,
Yawapi maringo yako, na hashuo za duniya,
Leo upo peke yako, sote tumekukimbiya

**Sasa ni chano cha mji**, watu wajichanatiya,
Umekwisha ujuwaji, haya zimekupoteya,
Yale usoyataraji, kwako yamekuhamiya.

**Bao la Mgahawani**, Kila mtu akaliya,
Julala huna soni, na wala sitara piya,
Wenyeji wote mjini, wamekwishakupitiya.

**Sasa jamvi la wageni**, wajapo huwapokeya
Imekutoka thamani, mtu duni mebakiya
Hata mbwa wa njiani, kukuona hukimbiya.

Kibwagizo:
Uwapi uzuri wako, yawapi maringo yako.

Katika shairi hili tamathali za semi zimebainishwa kwa wino mzito. Wanafunzi wanashauri kubainisha tamathali za Semi katika mashairi mengine yaliyomo katika diwani hii.

Mshairi wa **Fungate ya Uhuru** ametumia lugha ya picha na tamathali za semi ili kuongeza uzuri wa sanaa yake na kuwasilisha ujumbe aliokusudia kwa urahisi zaidi. Picha moja inaweza kudhihirisha wazo kwa uwazi zaidi.

Inafaa kusema hapa kwamba Muhamed Seif Khatib ametumia kwa ufundi mkubwa sana mbinu hizi za kisanaa za kutumia lugha ya picha na tamathali za semi.

## Mandhari

Mandhari ya mashairi haya yanaweza kuwa ni Afrika, ikiwa ni pamoja na Tanzania. Kipindi kinachohusika ni cha mara baada ya Uhuru hadi sasa. (1960 mpaka wakati uliopo).

Tunabaini hivyo kutokana na uhusiano wa visa vinavyosimuliwa na hali halisi ya Afrika. Matarajio ya wananchi walioshiriki katika kupigania uhuru bado hayajatimizwa. Wakati wananchi wakibaki hivyo viongozi wa Afrika wanaendelea kustarehe kwa kutumia jasho la wananchi.

Demokrasia kamili katika Afrika bado ni ndoto kwa muda mrefu. Umaskini ndiyo unazidi kujiimarisha na huduma za elimu na afya zinaendelea kuwa duni. Inaonekana kuwa kazi ya kutafuta maendeleo bado haijaanza kwani viongozi bado wako kwenye "fungate".

Kuendelea kwa "fungate" hiyo kunazusha malalamiko. Katika baadhi ya nchi hali hiyo imesababisha umwagaji wa damu. Hakuna haja ya mifano ya nchi kama hizo kwani zinafahamika dhahiri.

## Maudhui

### *Dhamira*

Mwandishi wa *Fungate ya Uhuru*, pamoja na mambo mengine, anakosoa tabia za baadhi ya viongozi wa serikali za Afrika za kuponda raha na kusahau dhamana waliyokabidhiwa na wananchi ya kuwaongoza kuelekea kwenye maendeleo waliyotarajia baada ya uhuru. Hivyo tunaweza kusema kwamba dhamira kuu ya diwani hii ni ukombozi.

Pamoja na dhamira hii kuna dhamira nyingine ndogondogo. Dhamira ndogondogo ni pamoja na: maadili ya maisha, mapenzi, na lugha ya Kiswahili.

Kutokana na hali hiyo tunaweza kuyagawa mashairi yaliyomo katika diwani hii kwa kuzingatia dhamira hizo.

***Mashairi ya siasa***

Mashairi ya siasa yanazungumzia masuala yahusuyo siasa. Kwanza mwandishi anampigia kampeni mgombea uraisi wa wakati ule Bw. Ali Hasan Mwinyi. kipindi kile kulikuwa na mfumo wa chama kimoja na mgombea wa kiti cha uraisi huwa anasimama peke yake bila mpinzani na kupigiwa kura ya ndiyo au hapana. Mwandishi anawasihi wananchi kumpigia kura ya kumkubali yaani kura ya **ndiyo** katika shairi lake la "Mwinyi Mumpe Ndiyo" (uk.35). Ingawa mwandishi anawasihi wananchi kumpigia Mwinyi kura ya ndiyo haelezi sifa za mtu huyo ambaye akichaguliwa atakuwa na dhamana kubwa ya kuliongoza taifa.
Pili, mwandishi anakemea tabia ya baadhi ya viongozi pamoja na wananchi ya kukariri mambo bila ya kutafakari na kuyaelewa. Kauli hii inajitokeza katika shairi lake la "Ukasuku"(uk.33-34). Kasuku ni ndege afugwaye ambaye ana uwezo wa kuigiza maneno ya binadamu bila ya kuelewa maana yake. Muhamed Seif Khatib katika shairi hilo anasema kwamba tabia hii ya ukasuku imerejesha nyuma maendeleo yetu. Anafafanua jinsi ukasuku unavyodumaza fikira za maendeleo. Hali ambayo mwandishi anaieleza kuwa ni akili muflisi, mawazo mepesi, na yasio na kasi, pamoja na vipawa vilivyodumaa. Kama ubeti ufuatao unavyoeleza:

Kupea kwa ukasuku
Rais huhubiri
Wabunge hukariri
Wasomi huhariri
Na taifa husimama.

Hoja hii ni ya msingi sana kwa sababu inapotokea hali ya kuvia kwa fikira na kushabikia mambo bila ya tafakari ya namna yoyote hakutakuwa na maendeleo ya aina yoyote kwa sababu ya kukosekana kwa mawazo mapya. Hata hivyo lalamiko hili la mwandishi linapingana na mwelekeo wake aliotuonyesha wa kutuhimiza kumpigia kura ya ndiyo Bw. Mwinyi ili awe rais wetu bila ya kututajia sifa zake. Mwandishi pia ameshindwa kuepuka ukasuku kwa kushindwa kuukosoa mfumo wa chama kimoja ambao ndio uliorutubisha tabia ya ukasuku anayoipinga. Hakuna ubishi kwamba mfumo wa chama kimoja ndio ulizuia kuchipua kwa mawazo mapya na kuendeleza ukasuku. Chini ya mfumo huo mtu hawezi kukubalika mpaka awe kasuku. Watu waliojaribu kukataa kuwa makasuku walionekana wahaini. Mwandishi angeutazama ukasuku kihistoria kuliko kuuchukulia kama ulivyo.

Tatu, mwandishi anafichua wizi wa mali ya umma unaoendelea kufanywa na watu waliokabidhiwa dhamana ya kusimamia mali hizo huku taifa likizidi kuangamia.

Mwandishi anabainisha hayo katika shairi lake la "Wizi"(uk.27-28). Anaongeza kuwa wizi umetapakaa katika jamii na taasisi zake zote. Taasisi hizo ni pamoja na za kiserikali, kidini, mashirika ya umma, na kwingineko. Mwandishi anasikitika kuona kwamba wizi huo unafanyika chini ya ulinzi wa vyombo vya dola vyenye dhamana ya kulinda mali hizo zisiibwe. Tutazame shairi lenyewe:

Wizi umo;
kanisani,
msikitini,
hekaluni,
Wanyang'anywao ni waumini.

Wizi umo;
ikuluni,
kasirini,
na bomani,
Wanyang'anywao ni fukarini.

Wizi umo;
viwandani'
mashambani,
maofisini,
Wanyang'anywao ni masikini.

Wizi umo;
magengeni,
madukani'
gulioni,
Wanyang'nywao ni watu duni.

Walinzi hawapo? La hasha!
polisi hulinda wezi,
majeshi huhalalisha wezi,
na dini zawabariki wezi.

Kilio hiki cha Muhamed Seif Khatib ni kielezo cha kuporomoka kwa mfumo wa maadili ya jamii na utawala wa sheria ambapo hata taasisi zilizo na jukumu la kusimamia haki na maadili zimekuwa mawakala wa kuwanyanyasa watu wanyonge. Hata hivyo mwandishi hakupendekeza hatua zozote za kubadili hali hii. Pengine anataka wananchi wajitambue na hivyo kudai haki zao. Lakini pia inawezekana mwandishi huyo ameogopa kutoa pendekezo ambalo linaweza kuwaudhi "wakubwa".

Ikiwa hivyo tunaweza kushawishika kusema kwamba mwandishi huyo ni mwanamapinduzi mwoga. Lakini kauli hiyo haimsadifu mtu aliyethubutu kubainisha uozo huo katika jamii na kuwasuta viongozi wa dini na wa serikali. Pengine alitaka wananchi watafute wenyewe suluhisho la matatizo hayo.

Mshairi pia anazungumzia misingi ya maendeleo ya umma. Anasema kwamba maendeleo ya umma ni pamoja na upatikanaji wa huduma muhimu za umma kama vile elimu, afya, na malazi. Aidha maendeleo ya umma hujumuisha ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi ya masuala yanayohusu maisha yao. Anasisitiza kwamba jamii ya watu walioendelea haina matabaka ya mabwana na watwana. Hata hivyo mtazamo huu kuhusu maendeleo ya umma una kasoro nyingi. Mwandishi anashauri kwamba dola litawahudumia watu kwa kila kitu jambo ambalo ni vigumu kulitekeleza kama ilivyokwishathibitishwa na historia. Ithibati hii ya kihistoria ndiyo inayotupa uwezo kutamka baadhi ya fikira za Muhamed Seif Khatib sasa zimepitwa na wakati.

**Ujumbe**

***Tuwe Wazalendo***

Mwandishi anasisitiza kuwa tuwe na mapenzi na nchi yetu. Kila aipendaye nchi yake yuko tayari kuipigania na kuiendeleza kwa nguvu zake zote ili kuiletea neema. Mwandishi anasema hayo katika shairi la "Nchi Yangu" (uk.6). Katika shairi hili mshairi anatamka wazi kwamba yeye amejitolea kuifia nchi yake. Hivyo kila mwananchi anatakiwa kuwa na moyo wa kujitolea kwa nchi yake.

***Viongozi wawe na ujasiri***

Mshairi anasema kwamba viongozi wasiwe waoga. Viongozi wanatakiwa kuwa majasiri. Kiongozi jasiri hukabili kazi hata kama ni ngumu na ya hatari. Anakemea tabia za baadhi ya viongozi ambao wanakuwa waoga kuchukua maamuzi na hivyo kushindwa kutatua matatizo ya wananchi. Anawafananisha viongozi wa aina hiyo na dakitari anayeogopa kumfanyia mgonjwa upasuaji na hivyo kumsababishia mauti. Mwandishi anayasema hayo katika shairi lake la "Mjamzito" (uk.8).

***Tusaidie ukombozi wa Afrika ya Kusini***

Mwandishi anahimiza ukombozi kamili wa Afrika kwa vitendo na kujenga ujamaa. Kwa mfano katika shairi la " Nikizipata Bunduki" (uk.12-13). Muhamed Khatib aliandika shairi hili wakati Afrika ya Kusini ikiwa chini ya mfumo wa utawala wa kibaguzi. Wakati huo Watanzania walikuwa na wajibu wa kushiriki kikamilifu katika kuwakomboa wazalendo wa nchi hiyo. Kwa hiyo mwandishi alikuwa

anawahimiza wananchi kwa kusema kwamba yeye akizipata bunduki atapambana na wabaguzi hao.

Mwandishi pia anasema kwamba akipata mamlaka, yaani bunduki, atawaangamiza viongozi ambao wamejipatia utajiri kwa kusaliti dhamana walizokabidhiwa na wananchi. Anasema kwamba angezitaifisha mali za viongozi hawa na kuwagawia wananchi walio duni. Aidha angetoa ajira kwa vijana ambao wamekuwa malaya na majambazi kutokana na ukosefu wa ajira.

Mwelekeo huu wa Muhamed Seif Khatib unaonekana kuwa wa kimapinduzi. Inawezekana mshairi huyu ameathiriwa na falsafa ya Karl Marx ambaye anasisitiza matumizi ya nguvu katika kuleta mapinduzi ya kijamaa.

*Tuache ukasuku*

Mwandishi anakemea tabia ya viongozi na wananchi kukubali kila kitu bila kufikiri. Hali hii ni dhalili na kikwazo kwa maendeleo. Mshairi anaeleza hayo katika shairi lake la "Ukasuku" (uk. 33 - 34). Anashauri kwamba viongozi, wabunge,na wasomi hawana budi kuondokana na ukasuku ili kuchanuza fikira za maendeleo. Hata hivyo mwandishi ameshindwa kufafanua ni kwa vipi fikira zinaweza kuchanua katika mfumo wa chama kimoja cha siasa anaoutetea. Katika mfumo huu "wimbo" bora ulikuwa ni "zidumu fikira za mwenyekiti". Kila mtu alipaswa kuimba hivyo. Lalamiko hili la mshairi kuhusu kukithiri kwa ukasuku katika jamii ni kielelzo dhahiri kwamba demokrasia ya kweli haiwezi kujengwa katika mfumo wa utawala wa chama kimoja cha siasa.

**Mashairi yahusuyo lugha**

Mshairi anaelezea kwa ufundi wa kisanaa jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kuwa na maneno yawezayo kubeba maana au fahiwati zaidi ya moja. Anaeleza hivyo katika shairi lake la "Dafina" lenye beti tisa. Tutazame mfano wa beti mbili kati ya hizo:

Paa, ni kuruka angani, Kama ndege na tiara.
Paa, ni mnyama porini, Ni mwenye nyingi papara.
Paa, ni kuteka mekoni, Moto uwake imara.
Paa, ni toa magambani, Samaki atiye sura.
Paa, pia ni la nyumbani, Makuti au karara.
Mgodi wa Kiswahili, Ni dafina isokwisha.

Kata, ni kulikata kuti, Kwa panga au kitara.
Kata, ni kunjiko la kati, Umbo la nyoka duwara.
Kata, ni kujitwika mti, Unajiwekea tambara.

Kata, ni kiponya mauti, Kiu inapocharura.
Mgodi wa Kiswahili, Ni dafina isokwisha.

Beti hizi mbili kati ya tisa za shairi hili ni uthibitisho mzuri kwamba Kiswahili kina utajiri wa maneno yanayofanana maumbo lakini yana maana tofauti. Hali hii inafanya Kiswahili kuwa lugha rahisi kutumiwa kisanaa kama alivyofanya mwandishi wa shairi hili.

**Mashairi ya mapenzi**

Mshairi anazungumzia mapenzi ya dhati na ya kweli. Anabainisha ubora wa mapenzi ya kweli na udhaifu wa mapenzi ya ulaghai. Mambo haya yanajidhihirisha katika mashairi ya "Wewe peke yako"(uk.49), "Nia yangu sigeuzi"(uk.50), na "U wapi Uzuri Wako" (uk.51). Katika "Nia yangu sigeuzi" mshairi anasisitiza mapenzi ya dhati yaliyo na staha. Katika pendo la namna hii kila moja humuenzi mwenziwe milele. Mshairi anamwomba Mungu awazidishie uaminifu huu kwani pendo la aina hii li tamu sana. Katika ubeti mojawapo wa shairi la "Nia yangu sigeuzi", mwandishi anasema:

Zamani limejengeka, wala halioti kutu,
Zuri linanawirika, pendo zuri hili letu,
Zinduna ambari yake, huo ni mfano wetu.
Nia yangu sigeuzi, kupenda anipendaye,
Ajue nitamuenzi, milele taishi naye.

Mwandishi anaendelea kusema kwamba pendo la kweli halilengi katika kumnufaisha mmoja wa wahusika. Aidha, anasema kwamba pendo la kweli lina huruma na uvumilivu. Mwandishi anatoa ujumbe mzito kwa jamii mamboleo ambayo ina ukame wa mapenzi ya dhati. Imekuwa jambo la kawaida siku hizi kusikia kwamba bwana fulani kakimbiwa na mke wake baada ya kuachishwa kazi. Vivyo hivyo si mara chache kusikia kwenye vyombo vya habari kwamba mwanamke fulani katelekezwa akiwa na mtoto mchanga. Taarifa kama hizo ni dalili na ushuhuda wa mapenzi ya ulaghai na ya uwongo baina ya wahusika. Kama kungelikuwa na mapenzi ya kustahiana hayo yasingetokea kama anavyoeleza mshairi katika beti mbili za shairi la "Wewe peke yako":

Ulimi fasaha, umeuzoeya,
Neno la karaha, hujanitoleya,
Hupendi madaha, ya kuniringiya.

Moyo wa huruma, na imani piya,
Hujui kuchuma, ni mwenye kinaya,
Na subira njema, unovumiliya.

Mwandishi pia anakemea uhuni na maringo. Katika shairi la "U wapi uzuri wako", tabia ya uhuni inakemewa sana kwa vile mwisho wake ni anguko na kukosekana kwa staha kwa mtu mwenye maringo. Anasema kwamba mtu mwenye maringo hukimbiwa na rafiki zake na kubaki peke yake. Katika ubeti wa kwanza wa shairi lililotajwa, mshairi anasema:

Uwapi uzuri wako, haupo umepoteya,
Yawapi maringo yako na hashuo za duniya,
Leo upo peke yako, sote tumekukimbiya.
Uwapi uzuri wako, yawapi maringo yako.

Pamoja na mtazamo mzuri wa mshairi kuhusu mapenzi kwa jumla kuna upungufu unaojitokeza. Mshairi ameelekeza mashambulizi yake kwa wanawake kwa ujumla. Vigezo vyote vya ubora wa mapenzi vinatumika kumpima mwanamke. Hakuna mahali ambapo wanaume wanajadiliwa katika jambo hili. Inaelekea mshairi ameathiriwa na mtazamo wa kijadi ambapo mwanaume haonekani kama anaweza kuwa na tabia mbaya. Maonyo yote kuhusu adabu njema huwa yanaelekezwa kwa wanawake tu. Ingawa mtazamo huu ulikidhi haja katika kipindi fulani cha kihistoria hauwezi kukidhi haja ya ulimwengu wa leo ambapo harakati za maisha zinawaweka wanawake na wanaume karibu kabisa kihadhi na kimahitaji. Haiwazekani, kwa mfano, kwa mwanaume kuona fahari kuwa "fahali wa kila mtamba". Hivyo, ingekuwa vyema kama mshairi angedhihirisha wajibu wa wanaume katika mapenzi.

**Falsafa ya Mwandishi**

Mwandishi wa diwani hii ameathiriwa na falsafa ya Karl Marx kwa kiasi kikubwa hasa katika matumizi ya nguvu. Mshairi anashawishi matumizi ya nguvu katika kuleta ukombozi kamili na kujenga ujamaa. Falsafa hiyo inajidhihirisha katika mashairi yafuatayo: "Nikizipata bunduki" (uk.12), "Gorila" (uk.16), "Ujamaa" (uk. 33), na "Ni vita si lelemama" (uk.38). Falsafa ya ki-Marx pia inajidhihirisha katika namna mshairi anavyoelezea mahusiano ya kijamii katika mashairi yake. Mshairi anabainisha matabaka ambapo kuna tabaka la walionacho wanaoneemeka kutokana na jasho la wanyonge walio wengi. Mashairi ya "Fungate" (uk.1), na "Wizi" (uk.27) yanathibitisha hoja hiyo. Pamoja na kuathiriwa na falsafa ya Marx Muhamed Khatib bado anaendelea kughubika utamaduni wa mwambao wa Afrika Mashariki ambao kwa kiasi kikubwa unahitilafiana na mwelekeo wa Karl Marx. Mathalani mshairi bado hajakana imani yake kwa Mungu na ana mtazamo hasi kuhusu mahusiano ya kijinsia hususan usawa kati ya mwanamke na mwanaume kama tulivyojadili katika mashairi ya mapenzi.